JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA
OFISIYARAIS
TAWALAZAMIKOANASERIKALIZAMITAA
HALMASHAURIYAMANISPAAYATABORA.

Anwani ya Simu"MKUU WA SHULE".
Simu nambari:+255262605404/0766598393/0752752438
Nukushi nambari:+255262605404
Barua Pepe:taboragirls@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA,
SANDUKU LA POSTA 152,
TABORA.

KUMB.NA.JI/TGS/177/ **Tarehe 28/11/2022**

JINA LA MWANAFUNZI.....
S.L.P.....
.....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA WILAYA YA TABORA MKOA WA TABORA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Kwanza,** katika shule hii mwaka 2023. **Shule ya Sekondari ya Tabora wasichana** ipo kusini mwa kituo cha mabasi chaTabora na stesheni ya reli, umbali wa km.3 toka stesheni ya reli na km.4 toka kituo cha mabasi Tabora Mjini kuelekea Kipalapala. Shule Imepakana na Sekondari ya Tabora Boys. Kutoka stesheni au Kituo cha Mabasi mjini unaweza kukodi 'taxi' kuja shuleni, nauli ni sh.5,000/= hadi 7,000/=.Aidha zipo Bajaji (Pikipiki za mataili matatu)nauli ni Tsh3,000/=, Pikipiki/bodaboda ni Tsh1,500/=, pia tunakutahadhalisha **kuepuka kufika usiku!**.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 09/01/2023 unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **07/01/2023**. **Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0756020660(MAKAMU MKUU WA SHULE).**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YA SHULE

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:-**

(i) Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi inayoishia kwenye kiwiko cha mikono na yasiyobana mwili.(Mashati ya mikono mirefu kwa wenye mahitaji maalumu(Wenye Ualbino)

(ii) Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni sidiria au vesti ziwe za rangi nyeupe au nyeusi, haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na hizi ndani ya shati la shule.

(iii) Sketi ya bluu bahari iliyokolea (kitambaa kizito cha suti) yenye mshono wa linda box kubwa mbele n a nyuma na malinda mawili kushoto na mawili kulia mbele na nyuma. Urefu wa sketi ufunike kifundo cha miguu.

NB:Zingatia rangi ya sketi kwa kuangalia vizuri picha iliyotumwa kwenye mtandao.

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi Jozi 2 vyenye kamba na visigino vifupi Jozi mbili(2).Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.

(v) Jozi tano za soksi nyeupe zisizo na mistari ya aina yoyote (free size/stocking) zinazofika magotini.

(vi) Wanafunzi wa Kiislamu, Nusu kanzu nyeupe mbili za kitambaa cha tetroni nzito na hijabu **(Juba)** nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua, zisizo na urembo wa aina yoyote na hijabu mbili nyeusi ndefu kwa ajili ya kushindia.

(vii) **Kwa ajili ya michezo:** Bukta ya njano, raban yeupe,T- shirt ya njano na sketi ya njano mshono wa solo kitambaa chatetroni.

(viii) Shamba dress (**Gauni)** mbili rangi ya dark bluu(kitambaa kizito cha suti) kwa ajili ya kushindia urefu ni **kufunika vifundo vya miguu** kwa dini zote, kwa wenye mahitaji maalumu (Albino) shambadress iwe na mikono mirefu. ***NB. Sare zote ziandikwe majina ya mwanafunzi.***

MISHONO YA SARE ZA SHULE.

Sketi ya darasani
(Blue bahari)

Sketi ya michezo
(Njano)

T-Shirt ya michezo
(Njano).

Gauni (Dark-blue).

Mbele

Nyuma

UNIFORM TABORA GIRLS SECONDARY

2.2 Madaftari 12 counter Books (Quire 4) dozen 1, kalamu za risasi na za wino,mkebe wa vifaa vya Hisa bati **(Mathematical set) na *Elemenatry learners Dictionary.***

Aje na Kadi ya Bima ya afya(NHIF)

2.3 Godoro size 2.5 'X6', Blanketi1,Chandarua nyeupe3'x6', shuka 3(mbili za Pinki na moja Nyeupe), foronya nyeupe moja na foronya ya pinki moja na mto mmoja.

Mahitaji mengine ya kibinadamu:

(i) Tranka kubwa1(sanduku la chuma) kwa ajili ya usalama wa vitu vyake na kufuri imara kwa ajili ya kufungia tranka.

(ii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko,kikombe na chupa ya chai).

(iii) Picha 4 passport size akiwa amevaa shatilashule(jeupe)na ziwe na "background"(kivuli) ya bluu nyuma.

(iv) Taulo,Vitenge au Kanga doti moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

(v) Tracksuit rangi ya kaki, Jozi moja yenye mistari myeupe au njano pembeni isiyo na kofia(atavaa wakati wa maandalio ya usiku)

(vi) Sweta la Light Blue lililofumwa kwa uzi mzito kwa ajili ya baridi,

(vii) T-shirt nzito ya shule rangi ya kijivu aina ya manga.

(viii) Viatu vya wazi (open shoes) kwa ajili ya kushindia.

KUMBUKA:
***Simu haziruhusiwi shuleni, hivyo kwa namna yoyote ile mwanafunzi asije na simu shuleni.**

*** Mwanafunzi analazimika kuvaa sare za shule wakati wote awapo shuleni, hivyo asije na nguo za nyumbani bali aje akiwa amevaa shamba dress au tracksuit.**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kw a Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Saya nsi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ya fuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shule ni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya shule wakati wote awapo shuleni.

(i) Kutunza maliza shule na kuzilinda ni jambo la lazima.

(j) Mwanafunzi analazimika kuhudhuria vipindi vyote vya dini kwa mujibu wa ratiba ya shule.

MUHIMU:

- Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa ***mama, baba,Mlezi, kaka au dada(ndugu wa tumbo moja/baba mmoja)tu*** na ***siyo ndugu mwingine***.T aarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi. Mwana funzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.

- Ni marufuku kuvaa kanda mbili wakati wa chakula katika Bwalo au mazingira yoyote ndani na nje ya shule, isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bwenini.

- Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka) siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita muhula wa kwanza na cha Nne kwa kuitwa na Uongozi. Wasifike shuleni endapo hawajaitwa na uongozi wa shule .

- Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwa wazazi/walezi wake, haruhusiwi kwenda kwa ndugu (Ubalozini) kipindi cha likizo fupi wala ndefu.

- Mzazi unatakiwa kuandaa pesa ya nauli ya kuja likizo fupi (kipindi cha Pasaka na Septemba)na likizo ndefu, mwezi Juni na Desemba na kuituma shuleni pindi tu itakapohitajika (utajulishwa ni lini utume nauli).
- Mwanafunzi harusiwi kuwa na urembo wa aina yoyote kama vile hereni, bangili, mkufu na pete za aina yoyote ile shuleni.
- Shule ni haturuhusu nywele ndefu hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja na nywele fupi na asinyoe mtindo wa aina yoyote ile.
- Mwanafunzi awapo shule atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa, ni marufuku mwanafunzi kulala au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa, akishindwa kuzingatia atafukuzwa shule.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Usagaji.
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli nakadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
9. Kuolewa ama kuwekwa kimada.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza, au kushiriki migomo na kuvuruga amani na usalama wa shule na usalama wa watu wengine.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kutoroka shuleni mchana au usiku.
14. Kuwa na simu ya mkono ni shuleni au kumiliki kifaa chochote kinachohusiana na simu(line, earphone, charger n.k).
15. Kuhama bweni alipopangiwa na kulala bweni jingine bila ruhusa.
16. Kunyoshea nguo bwenini/kutumia pasi ya aina yoyote bwenini.
17. Kuhamisha taa ya umeme(bulb)kutoka eneo moja kwenda kupachika eneo jingine.
18. Kubadili dini awapo shuleni tofauti na aliyoandika wakati wa kuripoti shuleni.

MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHI WA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Form for Medical Examination) ambayo itajazwa na Mganga mk uu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhi wa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo hayana kuyatekeleza kwa kikamilifu.

Njoo na vifaa vifuatavyo:-

1. Jembe na mpini wake-moja
2. Fyekeo-moja
3. Sicle (Kotama) -moja
4. Fagio za nje mbili
5. Ndoo (lita10) -mbili
6. Reki (rake–kifaa cha kuvuta uchafu) -moja
7. Dumu la lita tano lenye uwezo wa kutunza maji ya kunywa lita tano (matumizi binafsi) – moja.
8. Ream paper-mbili
9. Nakala ya cheti cha kuzaliwa. (Njoo na nakala moja ya cheti cha kuzaliwa).

Muhimu:- Tafadhali njoo na fomu hii yenye kurasa kumi na moja siku ya kuripoti shule ikiwa imejazwa na daktari ukurasa wa saba na nane.

MWL.LYDIAM.ELIUD
MKUUWASHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA
S.L.P. 152
TABORA

FORM NO.1

THE UNITED REPUBLIC OF

TANZANIA PRESIDENTS' OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL

GOVERNMENT FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I.

Pupil's full Name……

Age/Years……Sex……

Blood found (red and White)……..

Stool examination:……..

Urinalysis:……..

Venereal Diseases test:……..

T.B.test:……

EyeTest:……

Ears:……

Chest:……..

Spleen:……

Abdomen:……..

Urine for Pregnant:……

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment (s) e.g. arm, leg etc. Infection chronic or family disease etc.

……..

……..

Icertify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:……..

Designation:……..

Station:……..Date:……

Official Stamp:……

FORM NO.2

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI……..
2. TAREHE YA KUZALIWA…….MWEZI……..MWAKA……
3. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA……MKOA WA……
   ……..
4. KABILA……...
5. DINI……DHEHEBU……....
6. JINA LA MZAZI/MLEZI……
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…KIJIJI/MTAA……..
   KATA…… TARAFA……..
   WILAYA…… MKOA……..
   Na.ya simu……..
8. KAZI YA BABA/MLEZI……..
9. KAZI YA MAMA……....
10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe:Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
    ……..
    ……..
    ……..
11. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi(matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za Simu.Weka picha ya ndugu husika kwenye kiboksi kilichopo mbele ya jina lake.

(a) Ndugu……..
Uhusiano na Mwanafunzi……
Simu……..

(b) Ndugu……..
Uhusiano na Mwanafunzi……
Simu……..

(c) Ndugu……
Uhusiano na Mwanafunzi……
Simu……

……
SAINIYAMWANAFUNZI

TAREHE:…….. TAREHE:……TAREHE:……

FORMNO.3
MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…….....(jina kamili la Mwanafunzi) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pakujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo na ahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Nahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Na ahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfan o mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina la Mwanafunzi……..

Saini ya mwanafunzi……

Tarehe……

Shahidi

Jina kamili……

Saini…….

Tarehe…….

FORMNO.4

A: AHADI YA MZAZI:

Mimi……(jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……..Kidato cha ……Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shulehii. Na ahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wa ngu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Anuani kamili…….

Simu:……

Tarehe:…….